

**MKATABA WA UNUNUZI WA FRAME NA MILANGO KWA AJILI  
YA UKARABATI MEDICAL CLINIC KUWA CHUMBA CHA TIBA  
MTANDAO (TELEMEDICINE) KATIKA HOSPITALI YA RUFAA  
YA MKOA-IRINGA**

**KATI YA**

**MGANGA MFAWIDHI WA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA -  
IRINGA**

**NA**

**MANDELA FURNITURE COMPANY LIMITED**

**MKATABA WA UNUNUZI WA FRAME NA MILANGO KWA AJILI YA  
UKARABATI WA MEDICAL CLINIC KUWA CHUMBA CHA TIBA MTANDAO  
(TELEMEDICINE) KATIKA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA IRINGA** Sanduku  
la Posta 260 Iringa ambaye katika mkataba huu atajulikana kama Mwajiri kwa  
upande mmoja.

**MANDELA FURNITURE COMPANY LIMITED** ambaye katika mkataba huu  
atajulikana kama mwajiriwa kwa upande mwingine

**KWA KUWA** Mnunuzi anahitaji na yuko tayari kununua frame na milango vyenye  
thamani ya fedha shilingi 2,450,000/= sawa na mchanganuo umeambatanishwa na  
vifaaa vitaletwa ndani ya siku tatu(3) kwa ajili ya ukarabati wa medical clinic kuwa  
chumba cha tiba mtandao (telemedicine) katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Iringa

**HIVYO BASI** pande zote mbili zinashuhudia makubaliano yafuatayo:


1. **KWAMBA** Mkataba huu niwamauziano ya frame za mlango na milango kwa  
ajili ya ukarabati wa medical clinic kuwa chumba cha tiba mtandao.
2. **KWAMBA** Muuzaji atakuwa na wajibu wa kuuza vifaa hivyo kulingana na  
orodha ya vifaa vilivyoorodheshwa katika nukuu ya bei iliyoambatanishwa  
katika mkataba huu
3. **KWAMBA** Bei iliyonukuliwa katika fomu ya nukuu ya bei iliyoambatanishwa  
haitabadilika katika kipindi chote cha utekelezaji wa mkataba huu.
4. **KWAMBA** Muuzaji atakuwa na wajibu wa kutoa vifaa kulingana na orodha ya  
vifaa vilivyo katika fomu ya nukuu ya bei
5. **KWAMBA** Malipo yatafanywa baada ya vifaa kupokelewa na kukaguliwa  
kama ni timilifu na vinakidhi ubora unaotakiwa
6. **KWAMBA** Mkataba huu utafika kikomo baada ya vifaa kupokelewa na  
taratibu za malipo kukamilika
7. **KWAMBA** Muuzaji atakuwa na wajibu wa kufanya kazi kwa uaminifu na  
pasipo kumsababishia hasara yoyote mwajiri.
8. **KWAMBA** Mnunuzi au muuzajii atakuwa na wajibu wa kuvunja mkataba  
muda wowote atakapoona inafaa, pale atakapojiridhisha kuna ukiukwaji wa  
makubaliano katika mkataba


9. **KWAMBA** Mnunuzi atakuwa na wajibu wa kuvunja mkataba muda wowote atakapoona inafaa, pale atakapojiridhisha kuna ukiukwaji wa makubaliano katika mkataba
10. **KWAMBA** Endapo kutakuwa na hasara yoyote iliyosababishwa na muuzaji. Muuzaji atakuwa na wajibu wa kulipa gharama za hasara alizozisababisha au kukatwa malipo yake ilikufidia hasara iliyosababishwa
11. **KWAMBA** Endapo kama kutakuwa na ucheleweshwaji wa kazi uliosababishwa na muuzaji, mnunuzi atakuwa na wajibu wa kuvunja Mkataba
12. **KWAMBA** Mnunuzi atatoa kusudio la kuvunja Mkataba kwa maandishi ndani ya siku tatu
13. **KWAMBA** Mkataba huu ni halali kwa mujibu wa sheria za Tanzania na utatafsiriwa kwa mujibu wa sheria hizi.
14. **HIVYO BASI** Pande zote mbili zimeweka saini tarehe , mwezi na mwaka kama inavyoonyesha hapa chini:

Kwa ajili ya ushahidi wa makubaliano ya utekelezaji wa mkataba huu, pande mbili zinazohusika wameweka saini zao kama ifuatavyo:

**YAMESAINIWA NA KUTOLEWA NA**

Saini:..... 

Jina:..... 



Cheo: **MGANGA MFAWIDHI HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA-IRINGA (MNUNUZI)**

Tarehe: 23 - 05 - 2022

Saini : .....  ..... **HAKIMU MKAZI**  
IRINGA

Jina: ..  ..... **MKOBIA** ..

Cheo: **SHAHIDI UPANDE WA MNUNUZI**

Tarehe: 23 / 05 / 2022


**YAMESAINIWA NA KUTOLEWA NA**

Saini: ..... *Zahara Kihuelo* .....

Jina: *ZAHARA OMARY KIHUELLO*

Cheo: **MANDELA FURNITURE COMPANY LIMITED- IRINGA**

Tarehe; *23 / 05 / 2022* .....



Saini; ..... *Innocent Kilibika* .....

Jina: *INNOCENT KLIBIKA* .....

Cheo: **SHAIIDI**

Tarehe: *23 / 05 / 2022* .....

MCHANGANUO

S/N	DESCRIPTION	UNIT MEASURE	QUANTITY	UNIT PRICE	AMOUNT
1	HARDWOOD FRAMES				
	120 * 210 Cm	PC	1	375,000	375,000/=
	90 * 275 Cm	PC	1	425,000	425,000/=
2	HARDWOOD DOORS				
	115 * 205 Cm	PC	1	975,000	975,000/=
	85 * 210 Cm	PC	1	675,000	675,000/=
	GRAND TOTAL				2,450,000/=